

TAASISI YA SAYANSI JAMII (TASAJA)

REG.NO. S.A.19074

ANNUAL REPORT FOR YEAR 2013

JANUARY 2014

TABLE OF CONTENT

1.0 Introduction.....	1
2.0 The status of the association.....	1
3.0 Activities conducted	1
4.0 Financial affair.....	2
5.0 Conclusion.....	2

Annexure

1. The minutes of annual general meeting
2. Financial statement
3. Tasaja in the news

1.0 INTRODUCTION

This report is in compliance of the Societies Acts (2002) and the constitutions of TASAJA of 2013 and covers the status, the activities, and the financial affairs of the association as at the end of 2013

2.0 STATUS OF THE ASSOCIATION

TASAJA was registered on November 5th, 2013 and there are no changes as pertaining to change of address, name, office bearers, constitution and objective (s) of the association that was recorded in 2013.

3.0 ACTIVITIES OF THE ASSOCIATIONS

During the time under report TASAJA in the course of pursuing its objectives performed the following activities

3.1 Members' mobilization.

The management complied and contacted sociologist graduates and made them aware of the existence of the association with the view of luring them to seek membership in the association

3.2 Application for membership in the International Sociologist Association.

TASAJA applied for membership as a collective member in the International Sociologist Association which if admitted will facilitate sharing of information with ISA and other individual members.

3.3 Organization of cultural dances

TASAJA organized a cultural event involving traditional dances that was targeting the children and youth aiming at exposing them to our traditional values that seems not to be attracting them. The event planned in 2013 was however held on the new years of 2014. The outcome proved our worries and encouraged for more such event that would guarantees the revival of appreciation of our traditional values.



The young generation in action signifying that dances festivals are the assurances for the survival of traditional values(Tasaja)

3.4 Intervention in the issues Electronic Fiscal Devices (EFD)

Argued by our objectives to ensure harmonious relation and interaction among all parties in the society, TASAJA issued a press release advising the business community in Mwanza to end their strike and the government to find the possibility carrying the burden of supplying the EFD machines to the business community.(See annexure 3)

4.0 FINANCIAL AFFAIRS

Financial affairs were largely for meeting the institutional formulation and registration which was covered by members' donation. The full version of the financial affair is as shown in the accompanying financial statement.

5.0 CONCLUSION

Generally the report present the situation of the organization as required by the governing laws and regulation as well as the TASAJA's own constitution.

ANNEXURE 1: THE MINUTES OF ANNUAL GENERAL MEETING

TAARIFA YA MKUTANO MAALUMU WA TAASISI YA SAYANSI JAMII (TASAJA)

1.0 TAREHE YA MKUTANO: 21.01.2014

2.0 MAHALI MKUTANO ULIPOFANYIKA: Mgahawa wa Rest Africa Buhongwa

3.0 MAHUDHURIO:

Waliohudhuria (Tazama kiambatanisho)

NA.	JINA	CHEO	
1	Paul Mashimba	Mwenyekiti	
2	Abdul Mashauri	Makamu mwenyekiti	
3	Erasto Masawe	katibu	
4	Beatrice Thobias	Katibu Msaidizi	
5	Bituro Kazeri	Mwanachama	
6	Edwin Magongo	Mwanachama	
7	Emmanuel Ndomomondo	Mwanachama	
8	Mwanjombe Mukasa	Mwanachama	
9	Felister Ngonyani	Mwanachama	
10			
11			
12			
13			
14			
15			

Wasiohudhuria na sababu

1.Benadetha Mashala(Kwa Taarifa)

2.Erica Steven(Safarini)

3.Daissy Mbelle(Kwa taarifa)

4.Rita Leonard(Kwa Taarifa)

5.Lina Kabula(Kwa Taarifa)

6.James Kalekwa(Kwa Taarifa)

4.0 Kufunguliwa kwa mukutano

Mwenyekiti wa muda alifungua mukutano kwa kuwashukuru wajumbe waliofika. Baadaye alimkaribisha katibu kusoama agenda za mukutano.

Katibu alibainisha kuwa mukutano ulikuwa ni mukutano maalumu na agenda zake zilikua ni:

1.Kupitia taarifa ya mwaka ya taasisi

5.0 Majadiliano

5.1 taarifa ya mwaka ya taasisi

Wajumbe walipia taarifa ya mwaka ya Taasisi ya mwaka wa kalenda wa 2013 pamoja na taarifa ya mapato na matumizi na kuipitisha. Aidha waliagiza itumwe kwa wakati kwa mamlaka husika na wanachama.

5.4 Kufungwa kwa mukutano

Mwenyekiti alifunga kikao kwa kuwashukuru wanachama kwa michango yao na kutaarifu kuwa kikao kingine kwa mujibu wa katiba kitakua ni kikao cha robo mwaka kitakacho fanyika mwishoni mwa mwezi machi(Jumapili ya mwisho- 30.03.2014).

.....

MWENYEKITI

.....

KATIBU

ANNEXURE 2: FINANCIAL STATEMENT FOR THE YEAR 2013

INCOME

PARTICULAR	AMOUNT- TSHS	AMOUNT- USD
Membership fees	0.00	0.00
Membership annual subscription	0.00	0.00
Donation	150,000.00	0.00
Loans	0.00	0.00
Fine & penalties	0.00	0.00
Others	0.00	0.00
TOTAL INCOME	150,000.00	0.00

**LESS
EXPENDITURE**

PARTICULARS	AMOUNT-TSHS	AMOUNT-USD
Registration application fees	10,000.00	
Annual fees	140,000.00	
TOTAL EXPENSES	150,000.00	

BALANCES AS AT 31.12.2013

NIL

.....
MWENYEKITI

.....
KATIBU

Annexure 3: TASAJA IN NEWS

TASAJA YAJITOSA MGOMO WA WAFANYABIASHARA MWANZA.>>>



Afisa habari wa TASAJA, Bituro Kazeri aliyenyoosha mikono wakati akizungumza na wandishi wa habari jijini Mwanza.

TASAJA yajitosa mgomo wa wafanyabiashara Mwanza.

- *Yawataka wafanyabiashara warudi kutoa huduma kwa jamii.*
- *Yasema hoja waliyonayo wafanyabiashara ni ya msingi, lakini njia waliyoitumia sio sahihi.*

Na. Baltazar Mashaka.

TAASISI Sayansi ya Jamii (TASAJA) ya Jijini Mwanza, imeingilia kati mgomo wa wafanyabiashara ikitaka watafakari na kusitisha mgomo huo, kwa madai kuwa hauna tija kwa maslahi ya nchi na jamii.

TASAJA pia imewataka warudi kutoa huduma kwa jamii na serikali ibebe mzigo wa kusambaza mashine hizo kielektroniki ,Electronic Fiscal Device (EFD) kwani haitapoteza chcochote, ili kuondokana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mgomo huo.

Afisa habari wa TASAJA, Bituro Kazeri, akizungumza na waandishi wa habari jana Jijini Mwanza, alisema hoja ya wafanyabiashara hao kuhusu gharama kubwa za kununulia mashine za Ankara za kutolea kodi ni ya msingi, lakini njia waliyotumia ya mgomo, si njia sahihi ya kutatua matatizo bali ni kufungua mlango mwengine wa matatizo.

“Wafanyabiashara kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakinung’unika kupinga matumizi ya mashine maalum za Ankara za kutolea kodi (EFD) wanapouza bidhaa zao. Ununuzi wa mashine hizo umezua migomo na kuathiri huduma za kijamii na kiuchumi na kwa siku hizo ya serikali haikingiza mapato.

Mgomo huo utakuwa na madhara makubwa kwa jamii siku za karibuni,kama mishahara, ukosefu madawa hospitali na huduma zingine za msingi ”alisema Kazeri.

Alisema serikali pekee ikiachiwa mzigo huo wa kuagiza mashine hizo lazima gharama kubwa zitarudi kwa walaji na ni kuwabebesha mzigo mkubwa wa kodi. Lakini pia watumiaji wakiachiwa wazinunue kinachogomba ni upatikanaji wake.

“Sidhani kama tutafikia hatua mashine hazitatumika, na matokeo tunayotaka kwa njia ya mgomo hayataondoa hilo. Ndiyo maana TASAJA tunaitaka serikali irudi kule inakokopa ,ikiwezekana izungumze na benki ya dunia watukopeshe tununue mashine hizo tutalipa,”alisema Kazeri.

Aidha alisema wao TASAJA wanaunga mkono hoja za Serikali kuitia Mamlaka ya Mapato (TRA) kuwa matumizi ya mashine hizo yanalenga kupunguza mianya ukwepajji kodi na mianya ya rushwa miongoni mwa wakusanya kodi wasio waaminifu, kuongeza na kuboeresha ukusanyaji kodi na utunzaji kumbukumbu za mauzo na manunuzi .

Kazeri alidai kuwa teknolojia hiyo ya kutumia mashine za kutolea Ankara za kodi ikitumika vizuri, itaboresha ukusanyaji kodi na kuweka kumbukumbu sahihi zinazotiliwa shaka na maofisa wa kodi . Kwamba njia hiyo ndiyo inayotumika duniani kote na itaondoa manung’unico na lawama kati ya wafanyabiashara na watoza kodi.

“Mfumo huu ukiangaliwa kisayansi litakuwa ni jambo bora,Tunachokata ni upatikanaji wake.Ukinunua serikali itakulipa kuitia kodi unayopaswa kuilipa.Hii ni faida kwa serikali,wafanyabiashara na lazima watumiaji wafahamu faida zake na elimu ya matumizi ya mashine hizo za Ankara za kutolea kodi,”alifafanua Kazeri.

Alisema kuwa miradi mingi ya kuboresha ukusanyaji wa mapato nchini imekuwa ikipatya ufadhili wa Benki ya Dunia, hivyo ni vema Serikali ikaangalia uwezekano wa kufanya nayo mazungumzo au wahisani wengine ipate fedha za kununulia mashine hizo ni kuzigawa bila kujali ukubwa wa biashara.

Alisema matumizi ya mashine hizo kwa kiwango kikubwa yataiwezesha nchi kuongeza ukusanyaji kodi,kujenga na kukuza utamaduni wa kuchukua Ankara za mauzo na manunuzi ,ambao kwa hapa nchini ni wa kiwango cha chini na utajenga uhusiano mzuri baina ya wadau wa kodi ambao ni serikali,wafanyabiashara,watoza kodi na jamii.

“Kodi ndiyo uhai wa serikali na ustawi wa wananchi wake.Hakuna njia nyingine ya serikali kupata kodi mbalimbali bila kuwatoza wananchi wake kwa njia sahihi na uwazi mkubwa.TASAJA tunapendekeza matumizi ya mashine za kutolea Ankara ni njia muafaka ya kuleta ukusanyaji kodi sahihi na wa haki .Kila mdau anapaswa kuliunga mkono zoezi hili,”alisema Kazeri.

Wafanyabiashara wamekuwa wakituhumiwa kutumia vitabu viwili vya Ankara za kodi ,kutiliwa shaka kwa kumbukumbu zao za biashara na maofisa wa kodi hali ambayo imekuwa ikisababisha wakadirive kodi siyosahihi.

Kwamba TRA nao wanatuhumiwa kuwapandishia kodi wafanyabiashara katika makadirio ya kodi. Makadirio hayo makubwa yalikuwa yakijenga mazingira na njia ya kushawishi na kulazimisha rushwa,mambo yanayopingwa na wafanyabiashara.

Hata hivyo Kazeri alisema ujio wa mashine za kutolea Ankara za kodi ndiyo jibu muafaka la matatizo yanayouzingira mfumo wa ukusanyaji kodi na uhusiano kati ya wafanyabiashara na watoza kodi na ni njia ya kisayansi ya kushughulikia suala hilo.